

FIDI

KURASA

17



**NAKALA YA TAMTHILIA YA MWANGAZA
HADITHI KWA VIJANA WA MIKA 7 NAKUENDELEA**

UJUMBE

Kitabu hiki cha hadithi ni chapisho la Filamu fupi ya FIDI iliyoandaliwa kutokana na utafiti wa awali unaoakisi sintofahamu ya hali ya Usonji kwenye jamii uliofanywa kwa kushirikiana na wataalamu wa usonji Brenda Shuma na Ephraimand Antony kutoka Gabriella Rehabilitation Center iliyopo mkoa wa Kilimanjaro.

Maudhui ya filamu hii yaliandaliwa na Tai Tanzania, pamoja na wadau na wabobezi wa Usonji kama vile Hilda Nkabe (Lukiza Autism Foundation), Miriam Elisha (Buyegi Trust Fund) walioshiriki kataka hatua za mwanzo za ukusanyaji taafiti na simulizi zinazohusiana na Usonji.

Maudhui ya chapisho hili na filamu ya FIDI yamekusudia kutaarifu na kuhamasisha uelewa wa Usonji kwenye jamii ili kuondoa unyanyapaa uliokithiri kwa watu wenye usonji.

Walimu na wanafunzi pamoja na watoto wote kwa ujumla wanahamasishwa kutumia chapisho hili kuibua miadala na kuchochea fikra zinachangia katika kuondoa unyanyapaa juu ya usonji kwenye mazingira ya nyumbani, shuleni na kila sehemu ya maisha ya kila siku.

FIDI imedhaminiwa na Serikali ya Australia.

MUHITASARI

Kila mtoto anaupokee na umuhimu wake. Lakini katika jamii zetu, unyanyapaa unatufanya kuwaona watoto wengine kama hawana umuhimu. Hilo ndilo limemtokea mtoto FIDI, mwenye hali ya USONJI.

USONJI ni hitilafu inayotokea katika UBONGO na kuathiri mfumo wa fahamu na kumfanya mtoto kutokuwa na uwezo wa kuwasiliana na kuchangamana kama wenzake. USONJI unamkumba mtoto akiwa tumboni mwa mama na kuonekana dalili zake katika umri wa miaka miwili na kuendelea maishani mwake.

Kwa vile jamii haina ELIMU ya kutosha kuhusu USONJI, FIDI anapitia changamoto nyingi na kumfanya mama yake kutafuta mbinu za ziada kumpa nafasi ya kukua kwa uhuru kama watoto wengine.

FIDI ana aina ya USONJI unaomfanya kuishi kwa kujitegemea, pale atakapo pata msaada na mafunzo kamili ya kumwezesha kifikra. Changamoto ni kwamba, jamii yake inamkwamisha.


WATAYARISHAJI:

Tai Studio

MWANDISHI: PADILI A. JAMES

MCHORAJI: CHRIS KATEMBO

MSANIFU: VICTOR J. LYAMUYA



AMMMM!



TUPELEKE NA PIKIPIKI HOSPITALI, AENDELEE NA RATIBA ZAKE NA LEO MVUA KUBWA ZIMETANGAZWA.




SIJALI KAMA IPO WENYE RATIBA ZAKE. MPELEKE MWANAO HOSPITALINI.



TUKICHELEWA ITAKUWA TABU BABA FIDI.





ARGH!
NITAFANYAJE SASA
JAMANI.

KILA WIKI
ANATAPIKA,
SITAKI KUKUTA
MAITI YAKE
NDANI KWANGU.




VUUUUUM



FIDIII
UMETENGENZA NINI,
HEBU TUONE?



WEEEE!
HEBU TOKA HAPO,
UNATAKA UAMBUKIZWE
UKICHAA, UWE ZEZETA.



**FIDI TULIA BASI,
NGOJA TUANGALIE
RATIBA YA LEO.**

HAYA TULIA.






PICHA, MICHORO NA ALAMA, NI LUGHA AMBAYO FIDI ANAWEZA IELEWA, NA MAMA YAKE ALIKUWA AKITUMIA MICHORO KUWASILIANA NAE



ONAAA



UMEKUNYWA MAJI YA BOMBA SANA, UKAPATA MINYOO



USIPOENDA HOSPITALI, UTALIA NA MAUMIVU NA UTAKUFA, NITAKUPOTEZA MWANANGU.





OYA DOGO
TULIA BASI,
KELELE ZA NINI.

HEBU ACHA JIGONGA
GONGA KWENYE KITI.

MAMA
HEBU JITAHIDI
KUMSIMAMIA MWANAO,
ANATATIZO GANI?

MVUA KUBWA
INAKUJA, SITAKI
ITUKUTE HAPA.

MNADEKEZA SANA,
KISINDINO KIDOGO TU
VITA.

FIDI TULIA BASI,
FIDI ONAAA...
USIOGOPE.



LAKINI
DAKTARI..

SIO HILO TU,
NI MUHIMU WAGONJWA
WOTE KUHUDUMIWA KWA
STAHA NA UMAKINI HASA
WATOTO KAMA FIDI
WENYE USONJI.

NISIKILIZE
NESI..

IKWERA!

IKWERA
HIYO!

IKWERA!

SHWAAAAAAAAAAAA

MAMA
UNAENDA?



KWA SABABU YA MVUA KUBWA NA UPEPO MKALI, DARAJA LILIZIDIWA NGUVU NA KUKATIKA. HIVYO KUKOSA NJIA YA KUPITA.





KILA MTU ALITOKA NDANI YA DALADALA. NA KWA MBALI WALISIKIA SAUTI YA WANYAMA FISI WA MSITUNI.

KWA HARAKA ALIRUDI KWENYE DALADALA ILI WAVEZE KUTOKA HAPO WALIPO.



NA HAPO NDIPO MTI MMOJA MKUBWA UKAANGUKIA DALADALA KABLA YA DEREVA KUFIKA.



**WOTE WANASHANGAA NA KUKOSA MATUMAINI KABISA,
MAANA HAKUNA MAHALI PA KUKIMBILIA KWINGINE.**



**KATIKATI YA SINTOFAHAMU,
FIDI, ANAPATA WAZO
AMBALO LINaweza
KUWAKOMBOA KATIKA
CHANGAMOTO
WANAYOIKUMBA.**



**FIDI ANAKUMBUKA
KWAMBA ALIWAHI
KUBUNI JINSI YA
KUTENGENEZA CHELEZO
KAMA CHOMBO CHA
KUSAFIRIA MAJINI.**




WOTE WALIJKUSANYA KUANGALIA MICHORO YA FIDI.





KILA MMOJA ALIANZA KUWAJIBIKA
BAADA YA KUPATA MAELEKEZO YA
VITU VINAVYOHITAJIKA KUTOKA
KWA FIDI NA MICHORO YAKE ILI
KUTENGENEZA CHOMBO
KITAKACHOWEZA KUTEMBEA JUU
YA MAJI.



NA WAKATI HUO HUO,
FISI NAO WALIKUWA
WAKIZIDI
KUWAKARIBIA.



KWA MBALI, FISI NAO WALIANZA KUONEKANA.



FISI HAO
WANAKARIBIA
TUSUKUMENI
CHELEZO JAMANI.

SUKUMA!




BAADA YA JUHUDI YA KILA MTU, SASA WANATUMIA CHELEZO HILO
ILI LIWEZE KUWASAFIRISHA KWENYE MAJI NA KUOKOA MAISHA YAO.




HAYA..
TWENDENI HARAKA,
TWENDE!




WANAPATA MATUMAINI BAADA YA KUONA MAKAZI YA WATU KWA MBALI.








DEREVA NAE ALIKUWA NA MENGI YA KUSEMA
KWA WALIOMZUNGUKA NA KWA JAMII NZIMA PIA.







Australian Government



Tai

Storytelling for Social Change